# SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI WA MAPATO) YA 2016

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

1. Jina fupi na Kuanza Kutumika.

**SEHEMU YA PILI**

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA**

**KODI NAMBA 7 YA 2009**

2. Kusomwa.

3. Marekebisho ya Kifungu cha 18.

4. Marekebisho ya Kifungu cha 23.

5. Marekebisho ya Kifungu cha 54A.

6. Marekebisho ya Kifungu cha 56.

**SEHEMU YA TATU**

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO**

**LA THAMANI NAMBA 4 YA 1998**

7. Kusomwa.

8. Marekebisho ya Kifungu cha 16.

**SEHEMU YA NNE**

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI)**

**WA MAPATO NAMBA 9 YA 2015**

9. Kusomwa.

10. Marekebisho ya Kifungu cha 20.

**SEHEMU YA TANO**

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI**

**NAMBA 8 YA 2006**

11. Kusomwa

12. Marekebisho ya Kifungu cha 15

13. Marekebisho ya Kifungu cha 29

**SEHEMU YA SITA**

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI,**

**NAMBA 11 YA 2004**

14. Kusomwa

15. Marekebisho ya Kifungu cha 20

**SEHEMU YA SABA**

**MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI YA ZANZIBAR,**

**NAMBA 1 YA 2006**

16. Kusomwa

17. Marekebisho ya Kifungu cha 14

**SHERIA NAMBA 1 YA 2016**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**

**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**

**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

15th June, 2016

# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUBADILISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2016 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI NAMBA 7 YA 2009

Kusomwa.

**2.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 18.

**3.** Kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 18 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa neno "saba" na kuweka badala yake neno "kumi".

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**4.** Kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "walipakodi wote" na kuweka badala yake maneno "aina fulani ya biashara".

Marekebisho ya kifungu cha 54A.

**5.** Kifungu cha 54A cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza vifungu vidogo vipya vya (3), (4), (5), (6), (7), (8), (9) na (10) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

(3) Masharti ya kifungu hiki yatatumika kwa biashara yoyote inayoendeshwa chini ya uendeshaji wa biashara au mtu mwengine.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki:

(a) "kuendesha" inajumuisha kusimamia, kudhibiti au kuendesha biashara;

(b) "mmiliki" kuhusiana na bidhaa au mali itajumuisha, mbali ya afisa anayefanyakazi kwa nafasi yake, mtu yeyote ambae anayejitambulisha kuwa ni mmiliki, wakala, au mtu mwenye umiliki, au anayenufaika, au anayedhibiti, au mwenye uwezo wa kutoa au kusimamia bidhaa au mali.

(5) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki:

(a) mtu anayeendesha biashara anatakiwa, ndani ya siku kumi na nne kuanzia siku ya kusainiwa mkataba wa uendeshaji biashara hiyo aweke dhamana ya kutosha iwe ya fedha taslim au ya rehani kama itakavyoainishwa na Kamishna;

(b) Kamishna atakuwa na uwezo wa kuhaulisha dhamana hiyo kuwa mapato kwa lengo la kugomboa dhima ya kodi inayodaiwa kwa mtu huyo.

(6) Pale ambapo dhamana iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (5) haitatosha kulipa deni la kodi la mtu anayeendesha biashara, Kamishna anaweza, kwa lengo la kugomboa kodi, kuchukua dhamana iliyowekwa kati ya wahusika wanaofanya biashara hiyo, kama dhamana hiyo inahusisha mmiliki wa mali na mwendeshaji wa biashara hiyo.

(7) Mtu aliyeelezwa katika kifungu kidogo cha (5) hataondolewa majukumu yake ya kulipa kodi katika mamlaka yake ya uendeshaji na kitu au mali yoyote ya mmiliki au mtu anayeendesha biashara inaweza kuzuiwa na kutaifishwa kwa kulipia deni la kodi.

(8) Katika kutekeleza masharti ya vifungu vidogo vya (6) na (7) vya kifungu hiki:

(a) mmiliki ana jukumu la kutoa masharti au kutaka dhamana kwa mtu anayeendesha biashara kwa lengo la kulipa kodi, na kama mmiliki huyo atashindwa kufanya hivyo, atawajibika kulipa deni la kodi lililoachwa na anayeendesha biashara na mali zake zinazohusika na biashara hiyo zitaweza kutumika kulipia deni hilo;

(b) mtu anayeendesha biashara ni lazima atimize matakwa ya aya (a) ya kifungu kidogo hiki, na atakapokwenda kinyume na matakwa ya aya (a) ya kifungu kidogo hiki, biashara yake hiyo itachukuliwa kuwa anaiendesha kinyume na sheria na hatua muafaka za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

(9) Mmiliki wa mali analazimika kuwasilisha, ndani ya siku kumi na nne baada ya tarehe ya kusainiwa mkataba wa uendeshaji biashara, nakala iliyothibitishwa ya mkataba baina yake na mtu anayeendesha biashara kwa Kamishna na kumjulisha Kamishna si chini ya siku 30 kabla kusita mkataba kati yake na muhusika.

(10) Mmiliki atakayeshindwa kuwasilisha mkataba au kumjulisha Kamishna kusita kwa mkataba kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (9), atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa kiasi chote kinachodaiwa kama kodi na faini kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 15 cha Sheria hii.

Marekebisho ya kifungu cha 56.

**6.** Kifungu cha 56 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (2) mara tu baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1):

(a) Kamishna anaweza kuhukumu kosa lililofanywa na mtu yoyote chini ya Sheria hii, iwe mtu huyo amefanya maombi au hakufanya maombi, kwa kumtaka kulipa faini iliyoelezwa kwa kosa hilo;

(b) mtu ambae hakuridhika na hukumu ya Kamishna chini ya aya (a) anaweza kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Kamishna mbele ya Bodi ya Rufaa za Kodi."

(b) kuingiza maneno "na (2)" baina ya maneno "kifungu kidogo cha (1)" na "cha kifungu hiki" yaliopo kwenye kifungu kidogo cha (4) pamoja na kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki na kisomeke "kifungu kidogo cha (1) na (2)".

(c) kuvipanga vifungu vidogo vya (2), (3),(4), (5) na (6) na kuwa vifungu vidogo vya (3), (4), (5), (6) na (7) kwa mpangilio wake.

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAMBA 4 YA 1998

Kusomwa.

**7.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Namba 4 ya 1998 ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**8.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuvifuta vifungu vidogo vya (1), (2) na (4) na kuweka badala yake vifungu vidogo vipya vya (1), (2) na (4) kama vifuatavyo:

(1) Kwa madhumuni ya sehemu hii, "kodi kwenye manunuzi" maana yake ni:

(a) kodi iliyolipwa kwa usambazaji kwa mlipakodi aliyesajiliwa Zanzibar kwa bidhaa au huduma zinazotozwa kodi ambazo zitatumiwa na mlipakodi kwa lengo la biashara yake;

(b) kodi inayolipwa na mlipakodi kwa uingizaji wa bidhaa au huduma ambazo zitatumiwa na mlipakodi kwa lengo la biashara yake.

(2) Mlipakodi ataruhusiwa kukiweka kama deni kiwango cha kodi kwenye manunuzi yaliyotumiwa na mtu huyo ikiwa:

(a) bidhaa au huduma, ambazo kodi kwenye manunuzi imetumika zimepatikana Zanzibar na mlipakodi kwa lengo la kufanya usambazaji wa huduma au bidhaa zinazotozwa kodi;

(b) kwa upande wa uingizaji, mlipakodi amelipa kodi ya ongezeko la thamani inayotozwa kwa uingizaji chini ya Sheria hii;

(c) kodi ya ongezeko la thamani iliyozuiwa na wakala aliyeteuliwa kuzuia kodi katika kipindi maalum cha hesabu ambacho zuio limefanyika, na ambayo haijapunguzwa kabla;

(d) kodi ya ongezeko la thamani kwa usambazaji wa huduma, zilizolipiwa na mlipakodi kutoka sehemu yoyote nje ya Zanzibar zitakuwa ni kodi kwenye mauzo na kodi kwenye manunuzi ya mlipakodi, na mlipakodi huyo hataruhusiwa kuweka kama deni kodi kwenye manunuzi kwa huduma hiyo isipokuwa awe ameonesha kodi kwenye mauzo kwa kiwango sawa cha kodi ya ongezeko la thamani katika marejesho ambayo kodi kwenye manunuzi inadaiwa kupunguzwa.

(4) kodi kwenye manunuzi haitapunguzwa, haitawekwa kama deni au kudaiwa isipokuwa mlipakodi, wakati wa kuwasilisha marejesho ambayo ina punguzo au madai, awe anamiliki moja ya nyaraka zifuatazo:

(a) ankara ya kodi inayohusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma iliyotolewa chini ya Sheria hii;

(b) nyaraka za uthibitisho wa malipo kwa uwakala wa kuzuia kodi zilizotolewa chini ya masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi;

(c) nyaraka za forodha zilizothibitishwa na afisa anayehusika, zikiambatana na risiti ya malipo ya kodi inayodaiwa;

(d) risiti ya forodha na hati iliyosainiwa na Kamishna wa Forodha Zanzibar inayoeleza kiasi cha kodi kilicholipwa, iwapo bidhaa zimenunuliwa katika mnada wa forodha;

(e) uthibitisho wa hati ya uingizaji bidhaa iliyothibitishwa na afisa aliyeidhinishwa na ushahidi wa malipo yaliyofanywa, kwa huduma zinazoingizwa; au

(f) nyaraka yoyote ya ushahidi wa malipo kama Kamishna atakavyoeleza.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI WA MAPATO) NAMBA 9 YA 2015

Kusomwa. **9.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) Namba 9 ya 2015 ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**10.** Kijifungu cha kwanza kilichopo katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 20 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingizwa maneno "au malipo yanayolingana kwa Shilingi ya Kitanzania" baina ya maneno "USD 1" na "kwa mtu".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI NAMBA 8 YA 2006

Kusomwa.

**11.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mafunzo ya Amali Namba 8 ya 2006 ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**12.** Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kidogo kifuatacho:

"(4) Masharti ya kifungu kidogo cha (1), (2) na (3) hayatatumika kwa:

(a) Idara yoyote ya Serikali na Taasisi yoyote ya Umma ambayo haiendeshwi kwa faida na ambayo kimsingi inagharamiwa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali;

(b) Serikali za Mitaa;

(c) Afisi za Kibalozi; na

(d) Umoja wa Mataifa na Wakala wake.

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**13.** Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza kifungu kidogo cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) kila mwajiri atawasilisha kwa Naibu Kamishna ndani ya siku thelathini baada ya kumalizika kipindi cha miezi sita cha kalenda, taarifa ya miezi sita inayoeleza yafuatayo:

(a) malipo yaliyofanywa na mwajiri kwa kipindi ambacho kitahusika na malipo;

(b) muhtasari wa malipo yote na kodi iliyolipwa tofauti kwa waajiriwa wa kudumu na wasio wa kudumu pamoja na kodi iliyolipwa katika kipindi hicho;

(c) taarifa nyengine yoyote ambayo Naibu Kamishna ataihitaji";

(b) kuvipanga vifungu vidogo vya (2), (3), na (4) na kuwa (3), (4) na (5) kwa mpangilio.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI NAMBA 11 YA 2004

Kusomwa.

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi Namba 11 ya mwaka 2004 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**15.** Kifungu 20 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuweka namba upya kifungu cha 20(1) kuwa 20(1)(a);

(b) kuongeza aya mpya (b) na kuwa 20(1)(b) kama ifuatavyo:
"(b) Waziri anaehusika na fedha ataweka saini hati iliyotajwa kwenye aya (a) ya kifungu hiki".

(c) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka kifungu kidogo kipya kifuatacho:

"(2) Kwa lengo la kuimarisha uwekezaji, Waziri kwa kushauriana na kukubaliana na Waziri wa Wizara husika, anaweza kukubaliana na kuweka vivutio visivyo vya kodi, isipokuwa kwamba makubaliano yoyote yanayohusisha vivutio vya kodi yatafanyika kwa mashauriano ya pamoja na Waziri wa Fedha".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI YA ZANZIBAR NAMBA 1 YA 2006

Kusomwa.

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Rufaa za Kodi ya Zanzibar, Namba 1 ya mwaka 2006 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 14..

**17.** Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuondoshwa neno "Waziri" na kuwekwa badala yake maneno "Jaji Mkuu".

**Imepitishwa** na Baraza la Wawakilishi, tarehe 26 Mei, 2016.

**RAYA ISSA MSELLEM**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**